

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA

Telegram "AFYA", **DODOMA**  
Namba ya Simu: +255 26 2323267  
Nukushi No: +255 22 2138060  
Barua zote zitumwe kwa **Katibu**  
**Mkuu**



Mji wa Serikali – Mtumba,  
Barabara ya Afya,  
S.L.P 743  
**40478, DODOMA**

### TAARIFA KWA UMMA

Dodoma; Novemba 9, 2023.

Wizara ya Afya imepokea ujumbe unaosambaa katika mitandao ya kijamii ukionesha mteja anayepata huduma katika Kliniki za tiba na matunzo kwa watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (CTC) akitoa malalamiko kuhusu kauli zisizo za staha na kunyanyaswa na watoa huduma za afya wa CTC.

Wizara inakemea vikali vitendo vya utoaji wa kauli zisizo za staha na unyanyapaa kutoka kwa watoa huduma za afya, wateja wote wana haki sawa ya kupata huduma bora na ushauri wa kitaalam kutoka kwa watoa huduma za afya.

Vitendo vya Unyanyapaa na kauli zisizo za staha kwa wateja vinazorotesha utoaji wa huduma bora za matibabu. **Wizara inafanya uchunguzi wa tuhuma hizi na watakaobainika kufanya vitendo hivyo taratibu za uwajibishwaji zitafuata.**

Wizara inapenda kuwakumbusha watumishi wa Sekta ya Afya kuzingatia maadili ya taaluma zao na kutoa huduma bora za matibabu zenye staha, zinazojali utu, heshima, upendo, na uadilifu ili kuleta ufanisi katika upatikanaji wa huduma bora za matibabu nchini.

Wizara ya Afya itaendelea kutoa mafunzo ya Huduma kwa Wateja kwa watoa huduma za afya na kuboresha huduma za afya ili uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali ya Awamu Sita chini ya Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Sekta ya Afya uendane sambamba na ubora wa huduma za afya zinazotolewa.

Englibert Kayombo

**KAIMU MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**